

**JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA**  
**GATUZI NDOGO YA KANDARA - KIDATO CHA TATU**  
**KISWAHILI INSHA**  
Karatasi - 102/1  
Oktoba/Novemba - 2016  
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

- |   |   |
|---|---|
| <p>1. Hii ni barua kwa mhariri. Vipengele vikuu vya utungo wa aina hii; <u>maudhui na muundo</u> vizingatiwe.</p> <p>a) Muundo:<br/>Vipengele vifuatavyo vya kimuundo vijitokeze;</p> <ul style="list-style-type: none"><li>i) Anwani : ya mwandishi na ya mhariri.</li><li>ii) Mtajo : Bw/Bi mhariri, kwa mhariri, mhariri.</li><li>iii) Mada : Kwa herufi kubwa na ipigiwe mstari.</li><li>iv) Utangulizi : Aandike kwa kifupi na alenge mada moja kwa moja.</li><li>v) Mwili: Yaliyomo yajadiliwe na yafafanuliwe.</li><li>vi) Hitimisho: Ahitimishe kwa kutoa maoni ama mapendekozo kuhusu mada.<br/>: Aandike sahihi na jina lake.</li></ul> <p>b) Maudhui<br/>Mtahiniwa afafanue hoja zinazoonyesha <b>kuwepo kwa maovu kama vile</b>: Ufisadi, mauaji, unajisi, unywaji wa pombe haramu, wizi, utapeli n.k.</p> <ul style="list-style-type: none"><li>- Lazima ajadili hoja hizi na azitolee ufanuzi.</li></ul> <p>Tanbihi.<br/>Lazima mazingira yawe ya jimbo lake.</p> <p>2. Hii ni insha ya maoni. Vipengele vikuu vya insha vizingatiwe.</p> <p>a) Muundo.</p> <ul style="list-style-type: none"><li>- Utangulizi</li><li>- Mwiki</li><li>- Hitimisho.</li></ul> <p>b) Maudhui</p> <ul style="list-style-type: none"><li>i) Kuunga mkono.</li><li>- Huzitumia katika kudanganya katika mitihani.</li><li>- Wamepata uraibu na matumizi ya rununu na kuathiri masomo na kazi zao.</li><li>- Maadili yao yamezorota na kutokana na matumizi ya mitandao na kutazama filamu chafu.</li><li>- Huzitumia kuwatapeli watu.</li><li>- Zimewafanya kuzembea na kutowajibika kwa sababu wazitumia kwa muda mrefu.</li><li>- Wamezoea kuandika kwa usupi hivyo kuvuga lugha / sarufi. n.k.</li></ul> | <p>ii) Kupinga.</p> <ul style="list-style-type: none"><li>- Huwasaidia kielimu - kusoma na kufanya utafiti.</li><li>- Ni chombo cha burudani.</li><li>- Hutumiwa kuwasiliana na watu kutoka mbali.</li><li>- Anaweza kuhifadhi msahafu na kujikuza kiroho.</li><li>- Hupata habari kupitai kwa redia / runinga katika simutamba.</li><li>- Hurahisisha huduma za benki / kutuma pesa.</li><li>- Hutumiwa kupiga picha badala ya kununua video au kamera. n.k.</li></ul> <p><b>Tanbihi.</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>- Mtahiniwa anaweza kujadili upande mmoja. Anahitaji kufafanua kikamilifu angaa hoja <b>tano</b>.</li><li>- Watakaojadili pande mbili wafafanue angaa hoja tatu kuunga na mbili kupinga au tatu kupinga na mbili kuunga kisha waonyeshe msimamo wao.</li></ul> <p>3. Hii ni insha ya methali.<br/>Mtahiniwa abuni kisa kinachodhahirisha maana ifuatayo:</p> <ul style="list-style-type: none"><li>- Atupaye jiwe kuliko na watu wengi hawezি kujua litampiga nani. Si vyema kufanya kitu cha kuumzia wengi - Huenda katika kundi hilo ukamwumiza mzazi, nduguyo, mwanaao, rafikiyo n.k.</li></ul> <p>Tanbihi.</p> <ul style="list-style-type: none"><li>i) Kisa kiwe kimoja.</li><li>ii) Si lazima aeleza maana ya ndani na ya nje ya methali.</li><li>iii) Anayegemea upande mmoja tu wa methali amepungukiwa kimtindo.</li><li>iv) Atakayeandika kisa kisichohusiana na methali hii amepotoka kimaudhui.</li></ul> <p>4. Maneno kiini katika swalii hili ni kuwa akiielekea nyumbani na kusikia mayowe.</p> <p><b>Tanbihi.</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>i) Mtahiniwa atakuwa amepotoka kimaudhui iwapo kisa hakioani na kianzio.</li></ul> |
|---|---|